# MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU

## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KIDATO CHA KWANZA

**SEHEMU I - INSHA** **Alama 20**

Andika kisa kitakachoanza na maneno yafuatayo: kelele zilitanda usiku katika kijiji kizima …… Endeleza.

**SEHEMU II UFAHAMU** **(Alama 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali uliyoulizwa.**

Ni dhahiri kwamba uharamia umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika Mashariki. Taarifa za uharamia zimetawala vyombo vya habari, kiasi cha kwamba haipiti siku bila kuripotiwa visa vipya vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani. Matukio haya yamewalimbikizia maharamia na nchi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kutiwa kwenye mizani.

Yumkini tatizo hilo halitokei pasi na kumotishwa na kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu, suala hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mijini Nairobi na Daresalaam mnamo Agosti 7, 1998, na tukio la Septemba 11, mwaka wa 2001 kule Marekani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno kwa maharamia ni kutosheleza matakwa yao. Kwa upande mwingine, ukosefu wa tawala- wajibika katika maeneno kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingira yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelengwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umaskini na magonjwa yaliyosheheni pakubwa barani. Bila shaka, hili ni suala linaloshawishishwa na ‘kinyume mbele.’ Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri wa abiria na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaransa kunaelekea kupiga jeki juhudi zakukomesha uharamia ulimwenguni. Aidha, utawala wa nchi kunakochipuka uharamia haujajizatiti kuharamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa hali inayochangia upungufu na ucheleweshaji wa bidha muhimu zinazoendeleza ustawi wa uchumi. Dosari hii inaelekea kukwamiza majowapo ya maendeleo ya milenia yanasisitiza uimarishaji na ushirikiano wa maendeleo ya upanuzi wa masoko ulimwenguni. Harakati za kitalii katika kanda ya

Mashariki ya bara la Afrika zimehujumiwa. Na itakumbukwa bayana watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za mtandao ulimwenguni ni ndoto ambayo haijatimia hadi hivi sasa, kufuatia juhudi za maharamia katika bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa hali hii, mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni. Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyinginezo kwenye kanda ya mwambao zimetiliwa shaka si haba. Itabidi mikakati na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusitishwa.

**a) Kwa nini uharamia umetamalaki ulimwenguni? (alama. 3)**

1. Pesa au fidia walizolipwa maharamia.

2. Ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa.

3. Ukosefu wa utawala wa kuwajibika katika sehemu/nchi kunakotokea uharamia 3x 1 = 3

**b) Eleza madhara ya uharamia kwa jamii ya kimataifa. (Alama 2)**

Uharamia unaotokea barani Afrika umeelekezewa jamii ya kimataifa ambayo ni mhusika mkuu wa kuinusuru Afrika kutokana na njaa, magonjwa na umaskini 2x 1 = 1

Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri wa aabiria na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

**c) Uharamia unaelekea kumtia hofu mwandishi. Fafanua. (Alama. 3)**

i)Matumizi ya diplomasia na mashauriano hayajafaulu katika kumaliza uharamia uliwenguni.

ii) Matumizi ya nguvu yanaonekana kuendeleza uharamia.

iii) Utawala hanjajizatiti kuu haramisha uharamia

**d) Fafanua juhudi zozote mbili zinazofanywa na jamii ya kimataifa. (Alama 4. )**

1. Matumizi ya nguvu yanayohusisha mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka.

2. Matumizi ya diplomasia na mashauriano.

3. Kuharamisha uharamia.

**e) Eleza maana yafuatayo kwa mujibu wa kifungu.**

**a) Umechipuka -** Umetokea

**b) Dosari -** Kasoro /Kosa

**c) Harakati –** Shughuli

**III SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

**A) Taja irabu ya kati.** **(Alama.1)**

a

**b) Toa mifano miwili miwili ya aina za konsonanti konsontanti zifuatazo:** **(Alama 4)**

**(i) Vikwamizo**

f/v/thi/dh/s/z/sh/gh/h

**ii) Nazali**

**/m//n//ny//ng'**

**C) Kiimbo nini?** **(Alama 1)**

Mawimbi ya sauti mtu anaongeapo. Au

Kupanda na kushuka kwa sauti mtu anapoongea

Mtu anapoongea

**d) Weka shadda panapofaa.** **(Alama.2)**

**i) Mkuu** M'kuu

**ii) Kupatana** Kupa'tana

**e) Taja vipashio vitatu vya lugha.** **(Alama 3)**

sauti→ silabi→ neno

**f) Tambulisha aina mbalimbali za maneno katika sentensi ifuatayo.** **(Alama 5)**

**Mtoto yule ameingia ndani ya shimo.**

Mtoto – Nomino ( N) Yule – Kivumishi (V) amengia Kitenzi (J) ndani ya kihusishi (H),Shimo Nomino( N)

**e) Badilisha sentensi zifuatazo ziwe katika hali ya wingi.** **( Alama 4)**

**i) Papai hili lilinululiwa jana.**

Mapaipai haya yalinunuliwa jana.

**ii) Unyasi mrefu utakatwa kwa upanga.**

Nyasi ndefu zitakatwa kwa panga.

**f) Silabi ni nini? (Alama 2)**

Ni sehemu ya neno na hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja.

**g) Andika neno lenye muundo wa : (Alama 2)**

**i) I + I** au, oa, ua

**ii) K+ I+K+K+I** penda, lenga, rusha n.k

**h) Onyesha viwakilishi (w) katika sentensi ifuatayo. (Alama 2)**

**Wote wawili walimwona huyo.**

W- wote

W- huyo

**i) Kanusha sentensi zifuatazo. (Alama 4)**

**a) Yeye anaimba vizuri.**

Yeye haimbi vizuri

**b) Nyumba kubwa itajengwa**

Nyumba kubwa haitajengwa

**j) Tunga sentensi moja moja kutotautisha maneno yafuatayo. ( Alama 2)**

**a) Vua -** Ondoa nguo mwilini Mchezaji alivua nguo.

**b) Fua -** i) Safisha nguo kwa maji Mama anafua nguo

ii) Tengeneza kitu kutokana na madini - Mhunzi anafua chuma

iii) Ondoa makumbi kwenye nazi mgema anafua nazi

**k) Eleza maana ya semi zifuatazo: ( Alama 2)**

**i) Enda mrama**

Mambo kuharibika

**ii) Pata afueni**

Pata nafuu baada ya kuugua

**l) Onyesha kielezi ( E) katika sentensi ifuatayo:** **( Alama 1)**

**Nyanya alitembea polepole.**

Kielezi – Polepole

**m) Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi ya alama ya nukta pacha.**

Aonyeshe matumizi katika: o

i) Orodha

ii) Kuonyesha saa

iii) Katika tamthilia

iv) Kutenganisha mada kuu na mada ndogo

**n) Yakinisha sentensi ifuatayo.** **(Alama 2)**

**Maandishi yake hayaja mpendeza mwalimu**

Maandishi yake yamependeza mwalimu

**o) Nyambua vitensi vifuatavyo katika kauli uliyopewa mambanoni** **(Alama1)**

**Futa(tendeka) ½** Futika

**Chagua (tendea) ½** Chagulia

(alama 2)

**SEHEMU YA III : FASIHI SIMULIZI**

**a) Eleza majukumu matatu ya fasihi simulizi.** **(Alama 3)**

i) Kuelimisha
ii) Kuburudisha
iii) Kuelekeza
iv) Kuonya na kushauri
v) Kuukuza uwezo wa kufikiri
vi) Kuhifadhi historia
vii) Kututazamisha Mazingira yetu

**b) Taja vipera vinne vya fasihi simulizi.** **(Alama 4)**

i) Hadithi
ii) Maigizo
iii) Ushairi
iv) Semi

**c)i) Hekaya ni nini?** **(Alama 1)**

Ni hadithi  ambayo huwa na mhusika mmoja mjanja

**ii) Eleza umuhimu wa hekaya.** **(Alama 3)**

a) Hutoa maadili kwa wanajamii.

b) Hufunza watu kuhusu kutenda wema.

c) Husaidia wanajamii kutumia uwezo mkubwa wa kiakili  kujiokoa kutokana na dhuluma

d) Hufunza kwa katika ulimwengu uliojaa hila na shaka silaha ya maisha ni maarifa

**d) a) Hurafa ni nini?** **(Alama 1)**

Ni hadithi ambazo  huwa na wahusika wanyama ambao wana tabia sawa na binadamu.

**b) Eleza sifa tatu za hurafa.**

i) Wanyama hutumiwa kuwasilisha binadamu
ii) Huwa na funzo wazi
iii) Huwa na ujumbe wa kukejeli/kukosoa na kuelekeza
iv) Hupunguza makaly ya mguso kwa anayelinganishwa na mnyama

**IV) ISIMU   JAMII**

**a) Isimu jamii  ni nini?**

Ni somo linaloonyesha uhusiano uliopo kati ya lugha na  jamii (Alama 2)

**b) Taja kaida tano za lugha** **(Alama 4)**

1. Umri

2. Cheo cha mtu

3. Mada inayozungumziwa

4. rika

5. Hali ya mtu

6. Tabaka

7. Mazingira

8. Jinsia/ uana

**c) Eleza sifa nne za sajili ya hospitalini. (Alama 4)**

1.Huwa na mstamiati teule/maluumu kwa mfano : sindano, dawa, kipimo.

2. Kuna matumizi ya lugha rasmi kati ya mgonjwa na daktari

3. Ni lugha yenye maswali mengi na majibizano.

4. Huwa ni lugha yenye maelezo marefu hasa daktari akimwelezea mgonjwa kuhusu ugonjwa.

5. Kuna kuchanganya tarakimu za vipimo na maelezo.

6. Lugha ya unyenyekevu hutumika.

7. Lugha ya heshima pia hutumika